**RAUDHWA MODERN ISLAMIC PRE & PRIMARY SCHOOL**

P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA
RAUDHWA SCHOOLS

PHONE :+255789 588 152
+255758982224
+255767812235
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

# FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA MWAKA 2027

## A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI (Ijazwe kwa herufi kubwa tu)

**FOMU NA.** ________

| I. JINA LA MWANAFUNZI | | |
|---|---|---|
| JINA LA KWANZA | JINA LA BABA | JINA LA UKOO |
| | | |

PICHA YA MWANAFUNZI YA HIVI KARIBUNI

| II. TAREHE YA KUZALIWA | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU | MWEZI | MWAKA | NAMBA YA CHETI CHA KUZALIWA |
| | | | |

| III. HALI YA MALEZI YA MTOTO | | | |
|---|---|---|---|
| BABA NA MAMA | BABA TU | MAMA TU | HANA WAZAZI |
| | | | |

| IV. MAHALI ANAKOTOKA MTOTO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NCHI | MKOA | WILAYA | KATA | MTAA/KIJIJI |
| | | | | |

| V. JINSI | |
|---|---|
| ME | KE |
| | |

| VI. JE, AMEHUDHURIA SHULE YA AWALI? | |
|---|---|
| NDIYO | HAPANA |
| | |

| VII. UONI | |
|---|---|
| MZURI | HAFIFU |
| | |

| VIII. SHULE ALIKOTOKA MWANAFUNZI | | | |
|---|---|---|---|
| JINA LA SHULE | DARASA | MWAKA | NAMBA YA PREM |
| | | | |

| IX. TAREHE YA KUANDIKISHWA |
|---|
| |

| X. DARASA ALILOFIKIA | |
|---|---|
| DARASA | MWAKA |
| | |

| XI. Aina ya ulemavu: (AKILI, KUSIKIA, VIUNGO, NGOZI) | |
|---|---|



© 02 Dec 2025

## B. TAARIFA YA WAZAZI/WALEZI (Ijazwe kwa herufi kubwa tu)

| PICHA YA BABA MZAZI/MLEZI YA HIVI KARIBUNI | | PICHA YA MAMA MZAZI/MLEZI YA HIVI KARIBUNI | |
|---|---|---|---|
| **BABA MZAZI/MLEZI** | | **MAMA MZAZI/MLEZI** | |
| JINA LA KWANZA | | JINA LA KWANZA | |
| JINA LA KATI | | JINA LA KATI | |
| JINA LA UKOO | | JINA LA UKOO | |
| UDUGU | | UDUGU | |
| NA. NIDA | | NA. NIDA | |
| KAZI | | KAZI | |
| ELIMU | | ELIMU | |
| ANUANI | | ANUANI | |
| NA. SIMU | | NA. SIMU | |
| NA. WHATSAPP | | NA. WHATSAPP | |

| MAHALI ANAPOISHI MZAZI/MLEZI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NCHI | MKOA | WILAYA | KATA | MTAA/KIJIJI |
| | | | | |

## C. MATOKEO YA MTIHANI WA USAILI (KUJIUNGA)

| DARASA | CHEKECHEA, I & II | | | III – VII | | | WAST | DARAJA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SOMO | KSM | KAND | KUH | ENG | MATH | SCIE | | |
| ALAMA | | | | | | | | |
| DARAJA | | | | | | | | |

**Maoni ya mtaaluma**
(Ameshinda/Ameshindwa) ______________________________

**JINA:** __________________________________ **SAINI:** _________ **TAREHE:** ________



© 02 Dec 2025

## VIGEZO VYA KUCHAGULIWA

- **(i)** Kuanzia darasa la **kwanza** mpaka darasa la **pili**; Mwanafunzi atachaguliwa endapo atafikisha wastani wa alama **75/100** katika mtihani wa usaili.
- **(ii)** Kuanzia darasa la **tatu** mpaka la **saba**; Mwanafunzi atachaguliwa endapo atafikisha wastani wa **36/50** katika mtihani wa usaili
- **(iii)** Mwanafunzi ambaye hatofikisha wastani tajwa hapo juu atapokelewa kwa makubaliano maalumu kati ya mzazi na ofisi ya Mwalimu Mkuu kinyume na hapo hatochukuliwa.
- **(iv)** Mwanafunzi atapewa nafasi ya kujiunga na shule baada ya kukamilisha malipo ya ada na michango na mahitaji yote ya msingi awapo shuleni.
- **(v)** Mwanafunzi atakayechaguliwa kujiunga na shule hii atatakiwa kuripoti shuleni siku ya **Jumatatu tarehe 04 Januari 2027 kabla ya saa Kumi Alasiri**

## KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini, hivyo unatakiwa kuzingatia utaratibu, kanuni na sheria za shule ili shule iweze kuendesha shughuli zake za kila siku bila matatizo. Kanuni na taratibu za shule zinalenga kumpa mwanafunzi **UTII**, **HESHIMA** na **NIDHAMU** katika kusoma kwake.

1. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza.
2. Mwanafunzi ni lazima kuwahi shuleni pindi shule inapofunguliwa.
3. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule wakati wote wa shughuli za kishule ndani na nje ya shule.
4. Mwanafunzi ni lazima kuletwa na kufuatwa shuleni na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni katika siku, tarehe na muda uliopangwa akiwa amevaa sare ya shule iliyokamilika. Iwapo atachelewa kufika katika tarehe na muda uliopangwa hatapokelewa.
5. Ni lazima mwanafunzi kupimwa na kuleta **Medical Form** iliyojazwa na daktari kila ajapo shuleni baada ya likizo. Pia mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya lazima aufahamishe uongozi wa shule mara afikapo shuleni. Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitapokelewa na kutunzwa kwa mtoa huduma ya kwanza wa shule au mlezi anayehusika. Endapo mwanafunzi ana kadi ya bima ya afya anashauriwa kuja nayo na kuikabidhi kwa uongozi wa shule.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na simu, nguo za nyumbani, vipodozi, vyakula, madawa ya kulevya au kilevi (pombe) ya aina yoyote na kuvitumia, heleni, pete, bangili, perfume, radio, TV, ipad (na vifaa vingine vya kielectroniki), n.k.
7. Mwanafunzi haruhusiwi kuendesha gari, pikipiki, au bajaji ndani ya eneo la shule.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutoka/kutoroka kwenda nje ya shule aidha kwa kuruka uzio wa shule au kwa namna nyingine yoyote na kama ni muhimu shule itampeleka na kumrudisha. Mfano: Hospitali na siyo sokoni wala madukani.
9. Mwanafunzi harushusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum: staffroom (ofisi za walimu), ofisi za shule, jikoni, na nyumba za walimu na wafanyakazi wasio waalimu.
10. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria bila kukosa shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika kalenda ya shule, ratiba ya muongozo wa shughuli za kitaaluma (School Academic Schedule) na ratiba ya kila siku (School Daily Routine).
11. Ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele darasani, maktaba, mabwenini, parade n.k. pamoja na kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au vurugu/ugomvi utakaosababisha kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni. Hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
12. Ni marufuku mwanafunzi yeyote kujihusisha au kushiriki katika vitendo vya wizi wa namna yoyote awapo shuleni na anatakiwa kutunza mali za shule na vifaa vyake binafsi. Endapo atasababisha upotevu, au uharibifu wa aina yoyote ile wa mali za shule atatakiwa kulipa au kuleta mali hizo. Mfano; vitabu, n.k.
13. Mwanafunzi anapaswa kunyoa nywele katika namna ambayo nywele zake zote kichwani zilingane na ziwe fupi za kutumia kitana kidogo. Unyoaji usiofaa ambao ni pamoja na unyoaji wa panki,

denge na mitindo mingine yoyote inayofanana na hiyo, hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote awapo shuleni.

14. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kufanya usafi wa mazingira pamoja na usafi wake binafsi. Ni kosa kwa mwanafunzi kutupa taka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni pamoja na kumwaga taka zilizomo kwenye vyombo vya kutunzia taka kwa muda (dustbins) kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule. Ni marufuku kuchora picha kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitanda, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule n.k. Ili kudumisha afya njema mwanafunzi hapaswi kuchangia vyombo vya chakula na mwenzie wala kula kwenye kundi, asitupe hovyo mabaki ya chakula wala kutunza chakula muda usio rasmi kwa chakula, asifuge nywele ndefu, kucha na asipake kucha rangi.
15. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita katika eneo lisilo na barabara maalumu (trespass) ikiwa ni pamoja na kupitia madirishani.
16. Mwanafunzi ni lazima awe na heshima, adabu na utii katika nyanja zote. Asigomee au kukataa adhabu halali. Asitumie lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu na kwa watu wengine, asimame mwalimu, wafanyakazi wasio waalimu, mzazi au mlezi, mgeni au mtu anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani na kwenye ukumbi wa mikutano. Awaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake. Asivae mikanda mipana au yenye bakoli kubwa na isiwe na urembo (picha), suruali za mitindo kama vile modo na kuvaa mlegezo (sketi au suruali), kwahiyo mwanafunzi anatakiwa kuwa na nidhamu wakati wote awapo shuleni na nyumbani.
17. Ni kosa mwanafunzi kumdharau kiranja au viranja wa shule kwani kufanya hivyo ni kuwadharau walimu waliomkabidhi madaraka, hii ni kwa sababu viranja wanafanya kazi kwa niaba ya walimu na wanafunzi wote. Viranja wote waliochaguliwa hapa shuleni ni viranja wa shule nzima na wanayo madaraka kamili juu ya kila mwanafunzi bila kujali ni wa darasa gani au eneo gani. Heshima na utii ni vya lazima.
18. Ni kosa kwa wanafunzi kulala wawili au zaidi katika kitanda kimoja. Endapo mwanafunzi atabainika kufanya hivyo hatua kali za kinidhamu zitachuliwa dhidi yake, hii ni pamoja na kusimamishwa masomo.
19. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi au kukutwa kitu chochote kinachohusiana na mapenzi, mfano; barua, kadi, daftari la nyimbo za mapenzi na miziki, picha, n.k.
20. Mwanafunzi awapo hapa shuleni, ataendelea kuabudu katika dini/dhehebu la imani yake aliyotoka nayo nyumbani na inayokubalika na wazazi /walezi wake, hataruhusiwa kubadili dini/dhehebu akiwa shuleni isipokuwa kwa taarifa maalum ya mzazi/mlezi kwa uongozi wa shule endapo anampa uhuru mwanae kujichagulia kikundi cha kuabudia. Mawasiliano ya mahitaji mengine yoyote ya mwanafunzi vikundi au kikundi cha dini yatafanywa na kuwasilishwa kwa mzazi na mwalimu mkuu wa shule.
21. Wakati wa kurudi nyumbani kipindi cha likizo Mzazi/Mlezi atatakiwa kumfuata motto shuleni au atalipia nauli ya mwanae na gharama ya mlezi kutoka shuleni amsindikize nyumbani. Mtoto hatakabidhiwa kwa mtu amabaye uongozi haumtambui isipokuwa kwa maelekezo ya Mzazi/Mlezi.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule mara moja kama atachupa kwa makususdi mipaka ya shule kama vile

1. Kutosimamisha swala (waislamu TU).
2. Wizi.
3. Uasherati, Ubakaji, Ushoga na ulawiti.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
5. Uvutaji bangi
6. Makosa ya jinai.
7. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi.
8. Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
9. Kudharau Bendera ya Taifa. Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
10. Kuoa au kuolewa, kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi.
11. Kupata mimba au kutoa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
12. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.

 © 02 Dec 2025

13. Kukataa adhabu halali.
14. Kutofanya mitihani ya ndani na mazoezi.
15. Kutoroka shuleni.
16. Kumiliki simu ya mkononi ukiwa hapa shuleni
17. Kuingia kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni na katika kumbi za starehe.

## D. ADA, MICHANGO NA SARE ZA SHULE

### (i) Malipo ya Ada ya Shule

| ADA KWA MWAKA MZIMA (BWENI) |
|---|
| **1,700,000/=** |

**MCHANGANUO WA NAMNA YA KULIPA ADA KWA AWAMU NNE**

| AWAMU | KIASI CHA KULIPA |
|---|---|
| **1.** 30, Disemba 2026 | **600,000/=** |
| **2.** 30, Machi 2027 | **500,000/=** |
| **3.** 30, Juni 2027 | **300,000/=** |
| **4.** 30, Agosti 2027 | **300,000/=** |

### (ii) Michango ya shule

| Aina ya mchango | Mahafali | | Mitihani (Darasa la nne na saba) | Futari |
|---|---|---|---|---|
| | Darasa la 7 | Madarasa mengine | | |
| Kiasi | **100,000/=** | **50,000/=** | **100,000/=** | **60,000/=** |

### (iii) Sare ya Shule

| SARE ZA DARASANI NA NJE YA DARASA | |
|---|---|
| **WAVULANA** | **WASICHANA** |
| **275,000/=** | **250,000/=** |

**ZINGATIA:**

a) Sare za shule zinapatikana shuleni, malipo yapitie kwenye akaunti ya ada na michango tu.
b) Ada inaweza kulipwa yote kwa **awamu moja** au **awamu mbili** au kwa **awamu nne** kama ilivyoainishwa.
c) Michango yote ya shule inalipwa kwa pamoja awamu ya kwanza mwezi Januari 2027.

**MALIPO YA ADA, MICHANGO NA SARE YAPITIE BENKI ZIFUATAZO TU.**

Benki: **NMB**
Namba ya Akaunti: **51510043318**
Jina la Akaunti: **RAUDHWA MODERN ISLAMIC SCHOOL**

**AU**

Benki: **TCB (BENKI YA POSTA)**
Namba ya akaunti: **251405000014**
Jina la akaunti: **RAUDHWA MODERN ISLAMIC**

**AU**

Benki: **CRDB**
Namba ya akaunti: **0150001J01B00**
Jina la akaunti: **RAUDHWA MODERN ISLAMIC**


© 02 Dec 2025

# E. MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

## (i) Mahitaji Binafsi ya Darasani

| S/N | VIFAA | DARASA LA AWALI HADI DARASA LA 2 | DARASA LA 3 - 7 |
|---|---|---|---|
| | | IDADI | IDADI |
| 1. | Begi la shule | 1 | 1 |
| 2. | Daftari counter book (Quire 3) | - | 8 |
| 3. | Daftari madogo ya kawaida (Msomi) | - | 12 |
| 4. | Daftari mistari mikubwa na midogo (Page 200) | 6 | - |
| 5. | Daftari za vyumba/squared books (Page 200) | 3 | - |
| 6. | Daftari ndogo zisizokuwa na mistari (Page 200) | 3 | - |
| 7. | Faili (Spring file) | 2 | 2 |
| 8. | Kalamu za wino | - | 50 |
| 9. | Majaradio | 20 | 20 |
| 10. | Mathematical set | 1 | 1 |
| 11. | Mifutio (mikubwa) | 10 | 10 |
| 12. | Penseli za HB **(Box/Dazeni)** | 4 | 2 |
| 13. | Rangi za kuchorea **(Box/Dazeni)** | 2 | - |
| 14. | Ream paper A4 **(DOUBLE A)** | 2 | 2 |
| 15. | Rula (30 cm) | 5 | 5 |
| 16. | Vitabu vya TIE nakala 1 kila somo | 8 | 7 |

## (ii) Mahitaji Binafsi ya Bwenini

| VIFAA VYA USAFI | | | |
|---|---|---|---|
| NA | MAHITAJI | IDADI/KIASI | KILICHOLETWA |
| 1. | Dawa ya meno kubwa **Whitdent (Gramu 250)** | 4 | |
| 2. | Miswaki | 8 | |
| 3. | Dodoki la kuogea la kuvaa kiganjani (glove bath) | 4 | |
| 4. | Sabuni za kuogea (medicated soap) **DAZENI** | 4 | |
| 5. | Sabuni ya unga **kwa mwaka mzima kilo** | 15 | |
| 6. | Sabuni ya miche **(white wash au Jamaa au Family au Mkwano)** | 20 | |
| 7. | Dawa ya kung’arisha viatu **ya mkebe (Gram 80) kopo** | 8 | |
| 8. | Brashi za kuoshea viatu na za kupakia kiwi | 4 | |
| 9. | Mafuta ya ngozi ya mgando **(Grm 500) kopo** | 4 | |
| 10. | Kata kucha | 2 | |
| 11. | Beseni na ndoo ndogo | 2 | |
| 12. | Kopo la kuogea | 1 | |
| 13. | Mafuta ya nywele kwa wanaosuka kopo | 2 | |


© 02 Dec 2025

| VIFAA VYA NDANI BWENINI | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **MAHITAJI** | **IDADI/KIASI** | **KILICHOLETWA** |
| 14. | Godoro inch 4 - **DODOMA/SUPER BANCO** | **1** | |
| 15. | Shuka ya rangi ya pink | **1** | |
| 16. | Shuka ya rangi ya blue | **1** | |
| 17. | Blanket | **1** | |
| 18. | Chandarua cha mbu | **1** | |
| 19. | Sanduku la chuma (trunk) KUBWA na kufuri | **1** | |

| MAVAZI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **MAHITAJI** | **IDADI/KIASI** | **KILICHOLETWA** |
| 20. | Kanzu rangi nyeupe (**ME** aje akiwa amevaa) | **2** | |
| 21. | Baibui na juba rangi nyeusi isiyo na urembo (**KE** aje amevaa) | **2** | |
| 22. | Boxer za kiume **AU** Chupi za kike | **6** | |
| 23. | Taulo | **2** | |
| 24. | Vest / kaushi | **4** | |
| 25. | Mkanda wa kuvalia suruali wa ngozi na matundu (wavulana) | **1** | |
| 26. | Yebo za kuogea (**Pair)** | **2** | |
| 27. | Viatu vya wazi (Open shoes) isiyo yeboyebo. JOZI | **2** | |
| 28. | Soksi rangi nyeusi **(black) pair** | **8** | |
| 29. | Viatu vya michezo au raba rangi nyeupe | **1** | |
| 30. | Kitana au chanuo | **1** | |
| 31. | Nguo za kulalia (aje nazo) | **2** | |
| 32. | Viatu vya ngozi rangi nyeusi **(Pair)** | **2** | |

# F. MAMBO MUHIMU

## 1. Baada ya ukamilifu wa fomu:

Fomu baada ya kujazwa na kukamilika. Nakala moja irudishwe shuleni. Nakala ya pili ibakizwe kwa Mzazi/Mlezi/Mfadhili.

## 2. Nyaraka za kuambatanishwa:

i) Cheti /Matokeo ya kumaliza elimu ya awali
ii) Kwa wanaohamia awe na **PREM number** kutoka shule aliyokuwa anasoma.
iii) Nakala halisi za cheti cha kuzaliwa
iv) Vipimo vya afya vya daktari (Hospitali inayotambuliwa na serikali tu).



© 02 Dec 2025

## 3. Kiapo cha Mzazi/Mlezi

Mimi _________________ (**Mzazi/Mlezi**) wa _____________________________________ nimesoma kanuni zote tajwa hapo juu. Naahidi kuzifuata kanuni zote zilizowekwa na shule iwapo nitakubaliwa kujiunga na shule hii.

Jina la (**Mzazi/Mlezi**) __________________________________ Saini: ________ Tarehe: ________

**4.** Fomu hii itachangiwa Tsh **10,000/= (elfu kumi)** itakayokabidhiwa kwa aliyekupa fomu hii. (**Fomu iwe imesainiwa na kupigwa muhuli wa shule)**



**MKURUGENZI WA SHULE**

# *KARIBU SANA*

## <u>RAUDHWA MODERN ISLAMIC PRE & PRIMARY SCHOOL.</u>

***Tunamuomba Mola wetu atuongoze katika kheri na ailinde Shule yetu, Pia msitusahau katika swala na dua zenu.***

**MAWASILIANO**: Mkurugenzi **0767812235** Meneja **0769586152** M/Mkuu **0756259520**


© 02 Dec 2025

**RAUDHWA MODERN ISLAMIC PRE & PRIMARY SCHOOL**

P.O.BOX 166,
NYAKANAZI - BIHARAMULO - KAGERA

RAUDHWA SCHOOLS

PHONE :+255789 588 152
+255758982224
+255767812235
EMAIL : raudhwaschools@gmail.com

## STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM

*To be completed by a Licensed Medical Practitioner before admission*

### A. STUDENT INFORMATION

Full Name: ____________________________________________

Date of Birth: ____ / ____ / ______

Gender: □ Male □ Female

Grade/Class: ________________________

Parent/Guardian Name: ____________________________________

Contact Number: __________________________________________

### B. GENERAL PHYSICAL EXAMINATION

| Item | Findings | Remarks |
|---|---|---|
| Height | | |
| Weight | | |
| Body Mass Index (BMI) | | |
| Blood Pressure | | |
| Pulse Rate | | |
| Temperature | | |

### C. VISION & HEARING

Vision Test (with/without glasses): Right Eye ______ / Left Eye ______

Hearing Test: □ Normal □ Abnormal (Explain: _______________________)

### D. DENTAL & ORAL HEALTH

□ Normal □ Abnormal (Details: __________________________________)

### E. LABORATORY TESTS

| Test | Result | Remarks |
|---|---|---|
| Hemoglobin/Full Blood Count | | |
| Urine & Stool Examination (worms/schistosomiasis) | | |



© 02 Dec 2025

| Test | Result | Remarks |
| --- | --- | --- |
| Malaria Test | | |
| Hepatitis B & C | | |
| Tuberculosis Screening | | |
| HIV Test (optional, confidential) | | |
| Pregnancy Test (for female students) | | |

**F. IMMUNIZATION STATUS**

(Please tick or indicate date if completed)

□ Polio □ Measles □ Tetanus □ Hepatitis B □ HPV (if applicable)

Other vaccines received: ____________________________________________

**G. FITNESS ASSESSMENT**

□ Fit for school attendance

□ Fit with restrictions (explain: ……………………………………………………………………………)

□ Temporarily unfit (reason: ………………………………………………………………………………)

**H. DOCTOR'S DETAILS**

Name: ___________________________________________

Title/Position: ______________________________

Signature & Stamp: ________________________________

Date: ____ / ____ / ______

NOTE: This form must be submitted to the school administration before the student is officially admitted.



© 02 Dec 2025